


MWONGOZO WA AFYA YA MIFUGO



MWONGOZO WA AFYA YA MIFUGO

Elizabeth VanWormer, Abigail Ahmed, Alphonse Msigwa, Mwokozi Mwanzalila, Asha Makweta, Elizabeth Komba, Mira Kelada, and Rudovick R. Kazwala

Timu ya watafiti wenye ujuzi na taaluma mbalimbali kutoka mradi wa HALI ukishirikiana na wafugaji wanaoishi Kusini-Mashariki mwa Hifadhi ya taifa Ruaha waliweza kutambua na kuorodhesha magonjwa ambayo yanashambulia mifugo yao na hivyo kuandaa mwongozo huu kuhusu afya za mifugo. Abigail Ahmed, wa mtandao wa Afya Moja na mbunifu wa michoro kutoka Chuo Kikuu cha Nebraska-Lincoln, ndiye aliyebuni na kuchora michoro katika mwongozo huu na Kelly Kretchmer alichangia muonekano wa sehemu ya mbele ya mwongozo huu.

Tunawashukuru wafugaji wote kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Tanzania kwa ushirikiano wao na mrejesho waliotoa wakati wa kuandaa mwongozo huu. Vile vile tunawashukuru wafanyakazi wa mradi wa HALI na washirika wetu kwa kupitia na kutoa mawazo yao wakati wa kuandaa mwongozo huu kama vile: Deana Clifford, Christopher Gustafson, Mathias Matandala, Jonna Mazet, Jesca Mlawa, Hilda Mrema, Goodluck Paul, Zikankuba Sijali, Robert Sumaye, na David Wolking.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ufadhili wa watu wa Marekani kupitia Feed the Future Livestock and Climate Change Innovation Lab katika Chuo Kikuu cha Colorado na Idara ya utafiti wa kilimo ya Chuo Kikuu cha Nebraska-Lincoln.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



Feed the Future Innovation Lab
COLLABORATIVE RESEARCH { Adapting livestock systems to CLIMATE CHANGE }

HEALTH FOR ANIMALS AND LIVELIHOOD IMPROVEMENT PROJECT

HALI




UC DAVIS
VETERINARY MEDICINE
One Health Institute

UNIVERSITY OF
Nebraska
Lincoln


ONE HEALTH

TAARIFA ZA JUMLA




WANYAMA WENYE AFYA NA WAGONJWA

Wanyama wenye afya



- Imara na mkakamavu
- Ngozi laini na inayovutia
- Nywele zinazong'aa
- Anakula na kucheuwa chakula vizuri.
- Kinyesi kinakuwa na majimaji na ugumu kidogo
- Msafi sehemu zake za wazi kama mdomoni, puani, masikioni na sehemu za siri
- Hachechemei na anatembea kawaida
- Ute wenye uvyevu nyevu na rangi ya waridi
- Pua inayong'aa na yenye uvyevu
- Anapumua/kuhema kawaida
- Mkojo wa kawaida na wenye rangi ya njano
- Anatoa sauti ya kawaida: mfano akiwa anaunguruma


Wanyama wenye ugonjwa




- Amekonda
- Ngozi mbaya na isiyo na manyoya baadhi ya sehemu
- Nywele zilizolala, anazubaa na kusimama isivyo kawaida
- Anakosa hamu ya kula
- Kinyesi chenye majimaji au kigumu
- Mchafu sehemu zake za wazi, mfano mdomoni, puani, na sehemu za siri
- Anachechemea na kuyumba yumba akitembea
- Ute wenye rangi rani kama nyekundu, nyeusi, au zambarau
- Pua iliyokauka
- Kupumua isivyo kawaida
- Mkojo mweusi na wenye damu
- Kupiga kelele isivyo kawaida

NINI KINASABABISHA MAGONJWA?


Magonjwa yanayoweza kusambaa kutoka kwa wanyama kwenda kwa wanyama, mazingira kwenda kwa wanyama au binadamu yanasababishwa na vimelea vidogo. Baadhi ya vimelea vinaweza kuonekana kwa macho mfano minyoo katika vinyesi vya wanyama na vimelea vingine haviwezi kuonekana kwa macho bali kwa kutumia darubini. Kuna aina tofauti tofauti ya virusi, bakteria, fangasi, na wadudu wanaoweza kusababisha na kusambaza magonjwa kwa binadamu na wanyama. Hivyo tiba na kinga yake inatofautiana. Baadhi ya magonjwa husababisha vifo na mengine hudhoofisha afya za wanyama. Madaktari, wahudumu wa afya za wanyama wa jamii, na maafisa mifugo wamefundishwa namna ya kutambua vimelea na magonjwa mbalimbali na kutoa ushauri, tiba au kinga ili kuwa na wanyama na binadamu wenye afya.



Fangasi



Virusi




Bakteria


MAGONJWA YA MIFUGO

Njia za kueneza magonjwa

Kuna visababishi vingi vya magonjwa. Kumbuka, magonjwa yanayoweza kuhama kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu yanaweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa. Mfano: homa ya bonde la ufa.




Kugusana na mnyama mwenye ugonjwa



Kugusana na mtoto wa mimba iliyotupwa au majimaji yake



Kung'atwa na mnyama mwenye ugonjwa. Mfano: kichaa cha mbwa




Vifaa vilivyogusana na mnyama mwenye ugonjwa kama vile sindano, nguo, au viatu



Kung'atwa na wadudu kama vile mbu, ndorobo, au kupe



Baadhi ya magonjwa yanaweza kuambukizwa kwa kugusana na kinyesi, mkojo, damu, au majimaji yanayotoka kwa mnyama mwenye ugonjwa



Mazingira kama maji au malisho yaliyotumiwa na wanyama wenye ugonjwa



Kinga ya magonjwa ya mifugo

Endapo mnyama wako anatumwa, tafadhari muone afisa mifugo katika eneo lako. Serikali pamoja na mradi wa HALI hivi karibuni waliandaa warsha maalumu kwa ajili ya wataalamu wa mifugo na kilimo katika tarafa za Idodi na Pawaga na kuwafundisha mambo mbalimbali juu ya kutambua dalili za magonjwa, kutoa tiba na kinga. Afisa mifugo anaweza kukueleza vizuri juu ya madawa na chanjo ya mifugo yako.

Endapo utanunua au kupewa mnyama wa aina yoyote, hakikisha ya kwamba unamtenga na wanyama wenyeji kwa muda usiopungua wiki moja ili kuweza kujua kama ana ugonjwa au dalili za ugonjwa wowote.



MAGONJWA YANAYOWEZA KUTOKA KWA WANYAMA KWENDA KWA BINADAMU

Njia za kueneza magonjwa


Kuna magonjwa mengi ambayo yanaweza kuhama toka kwa mifugo kwenda kwa binadamu. Wakati mwingine ugonjwa mmoja unaweza kuwa na dalili tofauti tofauti kwa binadamu na wanyama. Mfano: ugonjwa wa kutupa mimba.



Kung'atwa na wadudu (mbu au kupe) mwenye ugonjwa.




Kunywa maji hayajachemshwa na yanatumia na wanyama pia




Kwa kula nyama mbichi au kuchinja mnyama mwenye ugonjwa



Kugusana na mnyama mwenye ugonjwa. Kunywa maziwa ambayo hayajachemshwa




Baadhi ya magonjwa binadamu anaweza kuyapata kwa kugusana na kinyesi, damu, hewa, majimaji, au mnyama mwenye ugonjwa




Kwa kugusana na mimba iliyotupwa au majimaji kwa mnyama mwenye ugonjwa

Jinsi ya kujikinga na magonjwa yanayoweza kutoka wanyama kwenda kwa binadamu




Chemsha maziwa na maji kabla ya kunywa (husani kwa matumizi ya watoto).

Osha mikono yako vizuri kwa sabuni na maji safi baada ya kutoka chooni, kushughulika na mifugo, na kabla ya kula chakula.




Jaribu kupunguza matumizi ya maji ambayo chanzo chake kinatumiwa na mifugo na wanyamapori kama inawezekana.

Ni muhimu kuhakikisha kwamba nyama unayotumia imekaguliwa vizuri na mtaalamu na kupikwa ipasavyo.



MAGONJWA KWENYE

**Ng'ombe,
Kondoo na
Mbuzi**



KUTUPA MIMBA

(M: IBIRUWOO, B: HOSMODA, S: KUTAJAA)



Kuvimba korodani

Kuvimba maungio ya miguu

Kuvimba chuchu

Kutupa mimba

Kuzaa mtoto mfu

Dalili


Kutupa mimba, kuacha kondo la uzazi, ugumba kwa madume, kuvimba kwa korodani, kuvimba kwa jointi na kuchechemea, homa za mara kwa mara, kupungua uzito, kupunguza kutoa maziwa.

Njia ya uenezaji

Mnyama kugusana na ndama aliyetupwa au majimaji ya ukeni. Vile vile kupandana.

Uenezaji kwa binadamu

Kunywa maziwa kutoka kwa mnyama aliyeathirika. Kutumia mkojo wa mnyama aliyeathirika. Kumsaidia mnyama wakati wa kuzaa bila kinga, mfano gloves.



Dalili kwa binadamu

Homa zisizokwisha, maumivu ya kichwa, kuumwa maungio ya miguu, mikono, na uti wa mgongo, mwili kudhoofika, kutoa mimba na ugumba kwa wanawake, kuumwa/kuvimba kwa korodani, kupungua uzito. Dalili zake zinaweza kuchanganywa na zile za malaria.



Kinga kwa wanyama

Tenga mnyama anayetaka kuzaa, safisha na fukia masalia baada ya kuzaa, choma au fukia kondo la uzazi au kitoto kilichotupwa, chinja wanyama wanaotoa mimba mara kwa mara, usichanganye mifugo kutoka makundi mbalimbali.



Namna ya kujikinga

Chemsha maziwa vizuri. Usitumie mkojo toka kwa mnyama anayetupa mimba. Tumia kinga wakati wa mnyama kuzaa.

HOMA YA BONDE LA UFA

(M/B: RIFT VALLEY, S: HOMA YA BONDE LA UFA)



Kutoka damu puani



Kutupa mimba



Kuzaa mtoto mfu

Dalili


Kutupa mimba mara kwa mara, homa kali, misuli kukakamaa, na shida kwenye kutembea, kutoka damu puani, kuharisha, wanyama wadogo (ndama) hufa kwa haraka.

Dalili za binadamu

Homa, kuuma misuli na kichwa, kichefuchefu na kuogopa mwanga, baadhi ya watu, ugonjwa ukiwa sugu huwa na vidoti vya damu katika ubongo na macho. Vifo vinaweza kutokea. Tiba: muulize daktari wa binadamu.

Kuenea


Mbu husambaza ugonjwa kwenye mifugo. Vile vile mbu wanaweza kusambaza ugonjwa mpaka kwa binadamu japokuwa watu wanaweza kupata ugonjwa kwa kugusana au kula nyama, damu, au maziwa na mnyama mwenye ugonjwa.



Tiba/Dawa

Ongea na bwana mifugo juu ya kutupa mimba mara kwa mara na dalili zingine.





Kuzuia katika wanyama

Pata chanjo kutoka serikalini. Usichanganye mifugo yenye na isiyo na ugonjwa.




Kinga (kwa watu)

Wasitumie damu, maziwa, na nyama mbichi kutoka wanyama wenye ugonjwa. Watu watumie vyandarua vyenye dawa.

MDOMO NA KWATO

(M: ORUKULUKU, B: SAREPTA, S: LUSOONA)



Vidonda mdomoni



Vidonda katikati na chini ya kwato



Kutoka mate kwa wingi




Vinundu kwenye chuchu

Dalili

Vidonda mdomoni, hususani juu ya ulimi na fizi, kutoka mate kwa wingi, vidonda katikati na chini ya kwato, kuchechemea, vinundu kwenye kiwele, kupungua uzito na uzalishaji wa maziwa, ndama hupuma kwa shida na kufa.


Njia ya uenezaji

Kugusana na mnyama aliyethirika (kamasi, mkojo, kinyesi), hewa, na vumbi. Ndama hupata ugonjwa kupitia maziwa.




Tiba/dawa

Muulize bwana mifugo.




Kinga

Tenga wanyama wanaoumwa. Usichanganye wagonjwa na wazima. Osha vidonda taratibu kwa maji yaliyochemshwa na kuchanganywa na majani ya ukwaju au asali.



NDOROBO

(M: ENDEROBO, B: GARETI, S: NDOROBO)




Dalili

Homa, kuvimba tezi, kutoka nywele mkiani, machozi, kupungua uzito, kupungua maziwa.

Njia ya uenezaji

Kutoka kwa ndorobo.




Tiba/Dawa

Ukianza kutibu mapema, kuna dawa. Ongea na bwana mifugo.

Kudhibiti/Kuzuia

Nyunyiza au mwagia dawa kuzuia kung'atwa na ndorobo. Jaribu kuzuia mifugo kwenda maeneo yenye ndorobo.



UGONJWA WA KWATO

(M: TINGISHI/SUPETA, B: ANG'ASHI, S: BUGIGA)



Vidonda chini ya kwato na katikati ya vidole

Kuchecheemea


Mbuzi kuchunga kwa magoti

Dalili

Vidonda chini ya kwato au katikati ya vidole, kuchecheemea, mbuzi huchunga kwa magoti, ugonjwa hutokea sana kipindi cha masika.

Njia ya uenezaji

Kupitia vidonda au michubuko iliyosababishwa na kuumizwa na miiba au mawe yaliyochongoka. Vimelea vya magonjwa hubaki katika matope/unyevunyevu na kisha kumpata mnyama. Asiyekuwa na ugonjwa.



Tiba/Dawa




Dawa nzuri zinapatikana. Wasiliana na bwana mifugo katika eneo lako.

Kinga

Usichanganye wanyama wagonjwa na wasio wagonjwa, usinunue mnyama anayechecheemea, epuka kuacha wanyama kwenye maeneo yenye matope, kausha na safisha zizi vizuri.

MINYOO

(M: IRIPODUKU, B: GRIRIGA, S: MAYOKAA)



Kuharisha

Kupungua uzito

Minyoo kwenye kinyesi


Manyoya yaliyofubaa

Dalili

Kuharisha, Kuvimba kwa tumbo, Kuwa mchafu, Ukuaji mbaya, Kupungua uzito, Kukosa hamu ya kula, Kukonda, Wakati mwingine minyoo huonekana kwenye kinyesi. Kupumua kwa shida (minyoo kwenye mapafu)

Kuenea

Kwa njia ya kula chakula kilichanganyika na kinyesi chenye mayai ya minyoo.



Tiba/Dawa


Dawa zipo na baadhi yake ni Albendazol, Levamisol, na Fenbendazol ambazo mnyama hunyweshwa kwa kipimo maalumu. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na bwana mifugo wako.

Kinga

Tibu minyoo kwa wanyama kila baada ya miezi 3.

MAGONJWA KWENYE

Ng'ombe



KIFUA KIKUU

(M: ENGEROGET NAYADO, S: PUMUU/MAPAFU)



Kuna aina mbili za kufua kikuu:

Kifua kikuu cha binadamu ambacho huenea kutoka kwa mtu mmoja mpaka mwingine. Kifua kikuu cha ng'ombe huu huenea kutoka kwa mnyama mmoja kwa mwingine na vile vile kwa binadamu.



Kukohoa



Kupungua uzito

Dalili (watu)



Kikohozi cha muda mrefu, wakati mwingine na damu, homa na kutoka jasho usiku, kupungua uzito na kujisikia vibaya, kuvimba tezi.


Dalili (wanyama)

Kikohozi cha muda mrefu, kupungua uzito, kukosa hamu ya kula, manyoya kulala, kupungua uwezo wa kutoa maziwa.

Kuenea

Hewa, kugusana, kunywa maziwa yasiyo chemshwa, kushika mzoga wa mnyama aliyeathirika, kula nyama mbichi ya mnyama aliyeathirika.





Tiba kwa binadamu

Nenda katika kituo cha afya ukapatiwe matibabu.



Kinga

Kama mnyama wako anakohoa kwa muda mrefu: mtenge na wanyama wengine, au chinja mnyama huyo chemsha maziwa ya ng'ombe na mbuzi kila mara.



MAPAFU

(M: ERIKPIU, B: CHAMBAFU, S: MAPAFU)




Kunyoosha shingo mbele



Kukohoa



Kupanua miguu




Dalili

Kukohoa, Kamasi (mafua), Kunyoosha shingo mbele, Kupanua miguu, Kupungua uzito, Kupungua maziwa.


Njia ya uenezaji

Hewa na kugusana.



Tiba/Dawa

Kuna dawa nzuri. Ongea na Bwana Mifugo. Pata chanjo kutoka serikalini.




Kudhibiti/Kuzuia

Fungia wagonjwa peke yao.




MAGONJWA KWENYE

Kondoo na Mbuzi



MAPAFU

(M: ERIKPIU, B: CHAMBAFU, S: MAPAFU)



Kunyoosha shingo mbele



Kukohoa




Kupanua miguu

Dalili

Kukohoa, kamasi (mafua), kunyoosha shingo mbele, kupanua miguu, kupungua uzito, kupungua maziwa.

Njia ya uenezaji

Hewa na kugusana.




Tiba/Dawa

Kuna dawa nzuri. Ongea na Bwana Mifugo. Pata chanjo kutoka serikalini.


Kudhibiti/Kuzuia

Fungia wagonjwa peke yao.



UGONJWA UPELE

(M: ERIRII, B: DAGHUTA, S: LUMEME)



Magaga kwenye mdomo



Magaga kwenye chuchu (kiwele)




Dalili

Magaga kwenye mdomo wa mbuzi/kondoo, magawa wakati mwinginie yanaweza kuwepo kwenye kiwele, kushindwa kula, kupungua uzito, vifo huweza kutokea kwa mbuzi/kondoo watoto.

Njia ya uenazaji

Kugusana na mnyama aliyeathirika



Dalili kwa binadamu

Magaga kwenye vidole/mikono, Huweza kupona bila tiba.




Tiba/Dawa




Dawa zinapatikana. Ongea na bwana mifugo katika eneo lako atibu magaga kwa Iodine. Unaweza kumpatia chakula laini mnyama endapo anapata shida kula. Wanyama wanaweza kupona bila tiba baada ya wiki 2-3.

Kinga

Usichanganye wanyama wagonjwa na wasio wagonjwa. Vaa kinga mikononi wakati wa kutoa tiba.




KIZUNGUZUNGU



Dalili za ugonjwa wa Kizunguzungu

Ugonjwa wa kizunguzungu una athiri mbuzi na kondoo na unaenezwa kupitia kinyesi cha mbwa mwenye minyoo. Dalili za ugonjwa kwa mbuzi na kondoo ni pamoja na kupindisha shingo, kuzunguka, kupiga kelele, kukosa hamu ya kula/kuchunga, kupungua uzito, kudhoofika kiafya na mwisho kufa.





Njia ya kueneza ugonjwa

Mbuzi/Kondoo wanaweza kupata ugonjwa huu kupitia Kinyesi cha mbwa chenye mayai ya minyoo. Mbuzi/kondoo wanaweza kula mayai hayo ya minyoo pindi wanapochunga na kuanza kuugua baada ya wiki hadi miezi kadhaa. Ugonjwa unaweza kuenea zaidi endapo mbwa watakula ubongo au viungo vya mbuzi/kondoo aliyechinjwa baada ya kuathirika na ugonjwa wa kizunguzungu.

Jinsi ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa

Fukia ua choma kwenye moto ubongo na mabaki mengine baada ya kuchinja mbuzi/kondoo ili kuzuia mbwa wasiweze kula.




Matibabu

Zungumza na afisa mifugo katika eneo lako kama una mbuzi/kondoo mwenye kizunguzungu. Mbwa wanaweza kutibiwa kwa kupewa dawa za minyoo kabla hawajaambukiza mifugo wengine. Hakuna dawa kwa mbuzi/kondoo kwasababu minyoo/ugonjwa huathiri ubongo.

MAGONJWA KWENYE

Kuku



KIDERI/MDONDO



Kulala chini



Kutoa maji maji machoni na puani



Uharo wenye rangi ya kijani



Kupooza miguu




Dalili

Kulala chini na, kutoa maji maji machoni na puani, kusinzia na kupumua kwa shida, uharo wenye rangi ya kijani, kukosa mwelekeo na kupooza miguu, kuvimba kifua na ngozi yenye madoa mekundu, kupunguza uwezo wa kutaga mayai, vifo vingi vya kuku. Lakini unaweza usione dalili zote kwa wakati moja.

Njia ya uenezaji

Kugusana na kuku wanaoumwa pamoja na kinyesi, maji maji toka puani, mdomoni na machoni. Binadamu anaweza kupata ugonjwa, japo sio kawaida na dalili zake ni pamoja na kuwasha macho.



Tiba/Dawa

Hakuna tiba, mweleze bwana mifugo juu ya vifo vya kuku.

Kinga

Chanjo inapatikana. Ongea na bwana mifugo kabla mifugo haijaanza kuumwa.



NDUI YA KUKU

(S: NDUI)



Vipele vya mviringo kwenye masikio na upanga


Dalili

Vipele vya mviringo kwenye masikio, miguu, upanga na sehemu zisizo na manyoya, husababisha kuku kuugua kwa wiki moja, kuku wanaweza kufa kwa ugonjwa huu.



Njia ya uenezaji

Kugusana na ndege anayeamwa.




Tiba/Dawa

Hakuna dawa, muulizea bwana mifugo namna ya kutibu vidundu.


Kinga

Hakuna chanjo, usichanganye kuku wazima na wagonjwa.



MAGONJWA KWENYE

Mbwa



KICHAACHA MBWA

(M: ORDIYA PAUKE, B: GESKA GUDEDA, S: LUSALOO-MBWA)



Ukali



Kutoka mate kwa wingi



Kushindwa kutembea vizuri




Dalili (kwa mbwa)

Wanyama wote wenye damu moto akiwepo binadamu wanaweza kupata ugonjwa huu ambao unaenezwa na mbwa.

Tabia zisizo za kawaida, Woga, Ukali/ukorofi/shari, Kumeza/kula kwa shida, Kutoka mate kwa wingi, Kushindwa kutembea vizuri, Kupooza. LAKINI mnyama anaweza kuambukizwa na kushindwa kuonyeasha dalili.

Kuenea

Kung'atwa/kulambwa na mbwa mwenye kichaa cha mbwa.




Hakuna matibabu kwa ajili ya mbwa



Tiba (kwa watu)

Osha kidonda haraka iwezekanavyo na sabuni na maji safi. Pata tiba haraka iwezekanavyo. Pata chanjo kutoka daktari.



Kinga

Chanja mbwa, epuka kung'atawa na mbwa, dhibiti mbwa wazululaji.



